


Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF, Audax Rukonge akiwasilisha mada kwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji mjini Dodoma hivi karibuni.

# Hasara ya kuuza korosho ghafi na umaskini kwa wakulima

Na **Veneranda Sumila**

TAKWIMU zilizopo hivi sasa zinabainisha kwamba asilimia mbili tu ya korosho zinasindikwa nchini. Sehemu kubwa ya korosho husafirishwa kwenda nje ikiwa ghafi na kuwanyima wakulima zaidi ya 300,000 thamani halisi ya zao hilo.

Tanzania ambayo ni ya pili kwa kilimo cha zao la korosho barani Afrika ikitanguliwa na Nigeria, pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji, sekta hii inakabiliwa na matatizo mengi ambayo kwa muda mrefu hayajatatuliwa. Ukosefu wa viwanda vya kusindika korosho umekuwa ni kilio cha wakulima ambao wamekuwa wakitegemea soko la nje kwa muda mrefu sasa.

Utafiti uliofanywa na Jukwaa la Kilimo linalohusisha asasi mbalimbali za kilimo (ANSAF) unaonyesha kwamba kuna haja ya kubadilisha sera haraka ili kuboresha kipato cha mkulima na kuongeza mchango wa zao hilo katika pato la taifa.

## Dola 110 milioni zinapotea kila mwaka

Katika utafiti uliofanywa mwaka 2008, ‘Mabadiliko ya kibiashara sekta ya korosho,’ uliofanywa na BEST AC na Technoserve ulionyesha kwamba kuna haja ya kuwapo kwa mabadiliko kwa sababu kuuza nje korosho ambazo hazijabanguliwa kumesababisha wakulima kuingiza kipato kidogo huku taifa likipoteza wastani wa dola 110 milioni kila mwaka.

Mbali na kuhitajika kwa mabadiliko hayo miaka mitano sasa imepita na hakuna mabadiliko yoyote yamefanywa huku pato la taifa kutokana na zao la korosho likiendelea kudidimia na kutokuwa la uhakika.

Kutokana na hali hiyo ni dhahiri mabadiliko ya kisera yangesaidia korosho kubanguliwa nchini na kuongeza thamani ya zao hilo.

Waraka mmoja wa ANSAF ambao uligusia njia za kuboresha sekta ya korosho nchini, umebainisha kwamba moja ya kikwazo kikubwa kinachosababisha korosho ghafi nyingi za Tanzania kuuzwa nje ya nchi, ni udhaifu uliopo katika sera, kukosekana kwa huduma za kifedha na mawazo finyu yanayoangalia zao hilo kwa kipindi kifupi bila kuangalia hali ya soko la kimataifa.

Akizungumza na gazeti la BusinessWeek kwa njia ya simu Mkurugenzi Mtendaji wa ANSAF, Audax Rukonge anasema Tanzania itafaidika na zao la Korosho endapo itajenga viwanda vya kubangua korosho ili kuongezea thamani ya zao hilo kabla ya kulisafirisha nje ya nchi.

“Korosho zetu zinatakiwa sana katika soko la dunia, kinachotakiwa kufanywa na serikali ni kushawishi uwekezaji kutoka kwa wazawa na hata wageni ili kujenga viwanda vipya vya kubangua korosho ili tusafirishe korosho zilizobanguliwa, tupate fedha zaidi za kigeni, na kubadili maisha ya wakulima wetu,” anasema Rukonge.

Rukonge anasema kama kutakuwapo na viwanda vya kubangulia korosho, uzalishaji katika kipindi cha miaka saba, utaongezeka kutoka tani 158,000 za sasa kwa mwaka mpaka tani 250,000.

Mbunge wa Liwale, Faith Mitambo anaamini kwamba kuwapo kwa viwanda vya kubangulia korosho, kutaongeza thamani ya zao hilo, kuwaongezea wakulima kipato, na kubadili maisha yao.

“Ni kweli nchi yetu ipo katika hali mbaya kutokana na kutokuwapo kwa viwanda vya kubangulia korosho, hali hii inawaumiza sana wakulima kwa sababu wanalazimika kuuza bidhaa zao zikiwa ghafi kwa bei ndogo, inayosababisha waendelee kuwa maskini,” anasema Mitambo.

Mshauri wa kimataifa wa kujitegemea na mwanaharakati ambaye amebobea katika zao la korosho kwa miaka 30 sasa, Jim Fitzpatrick, amesema tatizo lingine kwa Tanzania, ni kukosekana kwa mazingira bora ya soko la korosho nchini.

Amesema maeneo ambako korosho inabanguliwa, wakulima wamekuwa wakinufaika zaidi kuliko wale wanaosafirisha korosho ghafi katika soko la kimataifa.

**MIAKA SABA**

**Viwanda vitaongeza uzalishaji kutoka tani 158,000 za sasa kwa mwaka mpaka tani 250,000.**

**MWAKA 2007 NA 2012**

**Tanzania ilisafirisha korosho ghafi zaidi ya tani 461,000 kwa Dola 85 milioni za Marekani.**

**TAARIFA ZAIDI:**

**Nini kinastahili kufanywa ili kuwezesha uwekezaji wa korosho Tanzania**

1. Kushawishi uwekezaji katika viwanda vya kubangua korosho kwa kutoa mwanya zaidi kwa wawekezaji wazawa kupata fedha za uwekezaji huku wakishawishiwa kutengeneza ubia na wawekezaji wa kigeni.
2. Kutengeneza mfumo wa kubangua korosho na kusaidia upatikanaji wa bidhaa hiyo kutoka kwa wakulima na vyama vya ushirika.
3. Kutumia tafiti zilizopo kusaidia uwekezaji unaokwenda sambamba na upatikanaji wa mali ghafi.
4. Gharama za ununuzi kupitia vyama vya ushirika na minada ni kubwa na kusababisha kuwapo kwa ushindani katika sekta ya ubanguaji. Ni vyema gharama hizi zikaondolewa.
5. Kushawishi wabanguaji wadogo na wakubwa kufanyakazi kwa kushirikiana.
6. Kuwapatia tuzo wabanguaji wanaoendeleza wafanyakazi wao kupitia kodi na huduma za kisekta.
7. Uingizaji na uwekaji wa teknolojia ufanywe na serikali
8. kuondoa vizuizi katika biashara, rushwa,kutokuwapo kwa taarifa na jurasimu
9. Kuwa watu wanaojali sekta ya korosho.

## Pembejeo ni tatizo kwa wakulima

“Serikali ni vyema pia ikasaidia katika pembejeo, kuna ushahidi wa kutosha kwamba pamoja na serikali kutoa ruzuku katika pembejeo, bado zipo juu na pia inakua vigumu kwa mkulima kupata pembejeo halisi zinazohitajika na kwa muda unaotakiwa,” amesema Fitzpatrick.

Kati ya mwaka 2007 na 2012, Tanzania ilisafirisha korosho ghafi zaidi ya tani 461,000 kwa ‘gharama’ za dola 85 milioni za Marekani.

“Gharama hizi zingekuwa ni thamani ya mauzo kama wakulima hawa wangeuza korosho zilizobanguliwa nyumbani,” anasema Fitzpatrick.

Kwa mujibu wa ripoti, kuwapo kwa viwanda vya kubangulia korosho nchini, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kutaisaidia Tanzania kupata jumla ya dola 750 milioni za Marekani na kuleta mabadiliko makubwa kiuchumi Kusini mwa Tanzania ambako kunalimwa korosho kwa wengi.

Kwa mujibu wa Fitzpatrick, hivisa sasa mkulima anapata kati ya asilimia 57 na 65 ya bei ya mauzo ikiwa ni asilimia 15 chini ya bei ya mauzo iliyopangwa na Bodi ya Korosho Tanzania.

“Mauzo ya korosho nchini hayamsaidii mkulima kama ilivyo kwa wakulima wa nchi nyingine.

“Tukifikiria bei ya korosho nchini India, pato kwa mkulima wa Tanzania lipo chini sana, kipato cha mkulima wa Tanzania ni kidogo. Hii inatokana na ukweli kwamba kuna kodi kubwa, gharama kubwa za uzalishaji na usafirishaji wa kupeleka kwenye minada ya kimataifa. Ukiangalia yote hayo utabaini kuwa mkulima wa Tanzania hapati tija kwa zao lake analozalisha ukilinganisaha na wenzao wa Afrika Magharibi ambao wanauza katika soko la wazi,” inasema sehemu moja ya ripoti hiyo.

**Tujadiliane kupitia Ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako. Ujumbe wako mfupi ni Bure, hautozwi!**

**Ukurasa huu unadhaminiwa na BEST-AC na Mwananchi**